Usione Haya
(Don’t Be Ashamed)

Na

Alex S. Silvester

Usione Haya

Na

Alex S. Silvester

Novemba 21, 2017

Usione Haya

Ndugu tunapoishi katika ulimwengu huu kuna vitu vingi ambavyo tunavionea haya, lakini kuna kitu kimoja ambacho Mungu anatuambia tusikionee haya na hiyo ni Injili ya Bwana wetu Yesu Kristo. Kupitia injili tulizaliwa tena kwa sababu Mungu alimfufua katika wafu, na hicho ndiyo tunafundisha na kuhubiri; ni kifo, maziko na ufufuo wake.

Watu wengi hata wale wanaojiita "Wakristo" lakini sio, unaweza kuona kwamba wengi wa hawa wanakaa bila kufanya kitu au wanaionea haya injili ya Kristo. Wanawaonea haya hata wale wanaowazunguka, hawataki wajue kama wao ni wafuasi wa Kristo. Wanaionea haya kanisa na wanaona haya kutangaza kwamba ni kanisa lake ndio pekee alilonunua na kulitakasa kwa damu yake mwenyewe. Kanisa la Kristo, wale wanaoabudu kulingana na jinsi Bwana wetu alivyoagiza. Wameacha kuongelea vitu ambavyo sio sahihi na kuisimamia kweli.

Ni kwa nini watu wanakaa kimya? Kwa sababu wanaipendaa dunia na wanataka kuwa na watu wengi katika ulimwengu huu pia katika ulimwengu wa kidini. Wanahitaji kuwa maarufu na kukubaliwa. Wanataka watu ulimwenguni wawasifu hata kama wanafanya mema au mabaya. Hawataki kuwasikiliza wenye mawazo nyembamba na kushirikiana na wengi. Kuliko kuongea kwa ajili ya Kristo, polepole wanajichanganya na marafiki zao pamoja na majirani, na ndugu ambao sio wakristo, ili kwamba mtu asiwe na hisia dhidi yako. Tabia zao ni tofauti na ile ya Wakristo wa kwanza waliokuwa tayari kufa kuliko kumkana Bwana wao. Wakristo wa kwanza walifurahi kwamba walihesabika kuwa bora kushiriki mateso ya aibu kwa ajili ya jina lake. ***"Nao wakatoka katika ile baraza, wakifurahi kwa sababu wamehesabiwa kuwa wamestahili kuaibishwa kwa ajili ya Jina hilo. Na kila siku ndani ya hekalu na nyumbani mwao, hawakuacha kufundisha na kuhubiri habari njema za Yesu kwamba ni Kristo."*** (Mdo. 5: 41-42). Tunapaswa kutangaza jina lake kwa kuhubiri na kufundisha roho zilizopotea katika giza nene ya ulimwengu huu ulioharibika.

Tunafuata mafundisho na mifano ambayo Bwana wetu alituachia kupitia mitume wa neno lake. Mtume Paulo, "*Kwa maana siionei haya injili, kwa sababu ni uweza wa Mungu uuletao wokovu kwa kila aaminiye, kwa Myahudi kwanza na kwa Myunani pia. Kwa maana haki ya Mungu inadhihirishwa ndani yake, toka imani hata imani; kama ilivyoandikwa, mwenye haki ataishi kwa imani.*" (Rum. 1:16-17).

"*Maana kila mtu atakaye nionea haya mimi, na maneno yangu katika kizazi hiki cha uzinzi na dhambi, Mwana wa Adamu atamwonea haya mtu huyo, atakapokuja katika utukufu wa Baba yake pamoja na malaika watakatifu.*" (Rum. 8:38) Ilianza na Wayahudi alafu baadae tukalipokea kwa uelewa zaidi na ujuzi. Mtume Paulo ananukuu kile alichokisema Yesu; Mat. 21:42, "*Yesu akawaambia hamkupata kusoma katika maandiko, jiwe walilolikataa waashi, hilo limekuwa jiwe kuu la pembeni; neno hili limetoka kwa Bwana, nalo ni ajabu machoni petu.*" Yeyote anayemwamini hataionea haya injili yake naa hicho ndio tunafundisha. Aliuweka msingi wake nasi tunapaswa kupita juu yaa msingi huo tukiwaambia wengine kusudi halisi. Alilisema katika Agizo kuu. Mark 16:15-16, tunapaswa kufundisha na kuhubiri ili waweze kuamini na kuokolewa lakini kama tukiona haya kuwaambia dhambi zao na kutubu, wamepotea. Paulo alisema, "*Kama vile nilivyotarajia sana na kutumaini, kwamba sitaaibika kamwe, bali kwa uthabiti wote, kama siku zote na sasa vivyo hivyo Kristo ataadhimishwa katika mwili wangu; ikiwa kwa maisha yangu au ikiwa kwa mauti yangu.*" (Fil. 1:20). Kijana Timotheo aliambiwa hivyo ivyo na akaonywa asiionee haya injili. "*Basi usiuonee haya ushuhuda wa Bwana wetu, wala usinionee haya mimi mfungwa wake, bali uvumilie mabaya pamoja nami kwa ajili ya Injili, kwa kadiri ya nguvu ya Mungu; ambaye alituokoa akatuita kwa mwito mtakatifu, si kwa kadiri ya matendo yetu sisi, bali kwa kadiri ya makusudi yake yeye na neema yake. Neema hiyo tulipewa katika Kristo Yesu tangu milele, na sasa inadhihirishwa kwa kufunuliwa kwake Mwokozi wetu Kristo Yesu; aliyebatili mauti, na kuufunua uzima na kutokuharibika kwa ile injili; ambayo kwa ajili ya hiyo naliwekwa niwe mhubiri na mtume na mwalimu. Kwa sababu hiyo nimepatikana na mateso haya, wala sitahayari; kwa maana namjua yeye niliyemwamini, na kusadiki ya kwamba aweza kukilinda kile nilichokiweka amana kwake hata siku ile.*" (2 Tim. 1:8-12). Lazima tujifunze na kuonyesha tumekubaliwa na Mungu kama ilivyokuwa kwa Timotheo. (2 Tim. 2:15). "***Kwa kuwa ilimpasa yeye ambaye kwa ajili yake, na kwa njia yake vitu vyote vimekuwapo, akileta wanawengi waufikilie utukufu, kumkamilisha kiongozi mkuu wa wokovu wao kwa njia ya mateso. Maana yeye atakasaye na hao wanaotakaswa wote pia watoka kwa mmoja. Kwa ajili hii haoni haya kuwaita ndugu zake; akisema, nitalihubiri jina lako kwa ndugu zangu; katikati ya kanisa nitakuimbia sifa.***" (Heb. 2:10-12). Sababu ya injili.

Ndugu tunavyo vyote tunavyovihitaji katika maisha haya na wokovu. Hivyo basi, lazima tuwaambie wale wote ambao hawajaisikia kabla ya wakati kuwadia ambapo hakutakuwa na muda wa kufanya hivyo wakati utakapowadia; maandalizi yanahitajika na ni muhimu. Baba yetu hatuonei haya tunapomuita Mungu wetu. "*Lakini sasa waitamani nchi*

iliyo bora, yaani ya mbinguni. Kwa hiyo Mungu haoni haya kuitwa Mungu wao; maana amewatengenezea mji." (Heb. 11:16). "*Nanyi mwe na dhamiri njema, ili katika neno lile mnalosingiziwa, watahayarishwe wale wautukanao mwenendo wenu mwema kaatika Kristo. Maana ni afadhali kuteswa kwa kutenda mema, ikiwa ndio mapenzi ya Mungu, kuliko kwa kutenda mabaya. Kwa maana Kristo naye aliteswa mara moja kwa ajili ya dhambi, mwenye haki kwa ajili yao wasio haki, ili atulete kwa Mungu; mwili wake akauawa, bali roho yakee akahuishwa,*" (1 Pet. 3:16-18). Ndani ya kanisa au nje kunaweza kukawa na wale wanaokunenea mabaya hatakama utakuwa unafanya mambo mema lakini wanaona haya kwa sababu unalifanya kwa nia njema. "*Maana mtu wa kwenu asiteswe kama mwuaji, au mwivi, au mtenda mabaya, au kama mtu ajishughulishaye na mambo ya watu wengine. Lakini kwa sababu ni Mkristo asione haya, bali amtukuze Mungu katika jina hilo.*" (1 Pet. 4:15-16).

"*Basi kila mtu atakaye nikiri mbele ya watu, nami nitamkiri mbele za Baba yangu aliye mbinguni. Bali mtu ye yote atakayenikana mbele ya watu, nami nitamkana mbele za Baba yangu aliye mbinguni.*" (Mat.10:32-33). Kama tunaona haya hatuwezi kumkiri Kristo mbele za watu. Na hiki ndicho tulichofanya kabla hatujaenda katika maji ya ubatizo.

Rafiki yangu na nduguunasimaama wapi mbele za Bwana? je unamwamini au unamkataa? (Heb. 11:6; Yoh. 14:1). Hupaswi kuona haya, (Marko 8:38).

Amini na ubatizwe ili uokolewe kama hujafanya hivyo, (Mak. 16:16), au umeyakubali mafundisho ya wanadamu? Je wewe ni mshirika wa kanisa la Bwana (Mat. 16:18), na kwa hili namanisha wale wanaoabudu kulingana maagizo ya Bwana. au wewe ni mtu wa madhehebu yaliyoanzishwa na wanadamu? Je unalivaa jina la Kristo? (Mdo. 4:12), au unavaa jina la mwanadamu?

Kumbuka kwamba siku ya mwisho tutahukumiwa kwa neno la Bwana lenyewe (Yoh. 12:48). Tafadhali usimkatae Kristo na mapenzi yake. Usimwonee haya. mwamini, mtii, na umuishie, na siku moja atakukubali kama wake na kukupa uzima wa milele mbinguni.